SCHOOL BASED ASSESSMENTS SHUGHULI ZA KISWAHILI GREDI 2 MUHULA WA KWANZA 2023

KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA (ALAMA 5)
Mwalimu akuulize maswali yafuatayo ukijibu.

1. Unapenda mnyama gani.
2. Kwa nini unampenda mnyama huyo?
3. Taja jinsi unavyomlea mnyama wako.
4. Eleza umuhimu wa mnyama unayempenda.
5. Mnyama unayempenda ana miguu mingapi?

KUSOMA KWA SAUTI (ALAMA 10)
Darasa Letu huwa safi kila wakati. Wanafunzi wote huhusika katika kulisafisha darasa letu. Mwalimu wetu wa darasa ametupanga kila mtu na siku yake ya kusafisha darasa. Tunapenda mazingira safi.Tuko na pipa darasani. Sisi hutupa taka kwenye pipa hilo kisha mmoja wetu hupeleka uchafu huo kwenye Jaa pindi lijaapo. Sote tunajua mazingira safi ni afya bora. Hatutaki kuugua. Tunapenda mazingira safi.

Ufahamu (Alama5)
Nuru anapenda chakula, Yeye ana afya nzuri. Mamake Nuru hupika vyakula vya kila aina. Hivi huhakikisha Nuru anapata lishe bora ili aepuke magonjwa mbalimbali. Mama yake Nuru hupika vyakula kama vile wali, ugali, mchicha, kabeji, samaki, nyama na maboga. Yeye pia huhakikisha ameandaa sahani ya Matunda ya kila aina. Matunda hutusaidia kukinga mili yetu dhidi ya magonjwa.

1. Nuru anapenda nini
2. Kwa nini mama humpikia Nuru chakula chenye lishe bora.
3. Andika vyakula vitatu anavyopika mamake.
4. Taja mboga tatu zilizotajwa kwenye kifungu.
5. Matunda hutusaidia vipi mwilini?

Sarufi (Alama20) Andika wingi wa sentensi zifuatazo.

1. Mgeni alichelewa kufika.
2. Ng'ombe alitibiwa mguu.
3. Mbona unapenda kusoma?

Chagua neno mwafaka la kujaza mapengo.

4. Mgeni anapoondoka akisafiri yeye hutuaga (kwaheri, masala)
5. Mwalimu hutuamkua (asante, shikamoo) anapofika asubuhi.
6. Unaporudishiwa kitu ulichopoteza utamwambie aliyekurudishia (Marahaba, Asante)
7. Sabalkheri ni salamu ya wakati upi?(Jioni, Asubuhi)